**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**TUME YA UTUMISHI SERIKALINI**

## TANGAZO KWA WATUMISHI WA UMMA

**YAH: TAARIFA YA KUKANUSHA KUHUSU UHAKIKI WA MAJINA NA TAARIFA ZA WATUMISHI WA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR INAYOSAMBAA KATIKA MITANDAO YA KIJAMII.**

Tume ya Utumishi Serikalini inawaarifu watumishi wote wa umma kuwa kuna taarifa ya uhakiki wa majina na taarifa za watumishi inayosambaa katika mitandao ya kijamii inayowataka watumishi walioajiriwa kuanzia 2000 kwenda kuhakikiwa.

Tume ya Utumishi Serikalini inakanusha kuwa haifanyi uhakiki wa watumishi hao na inawataka watumishi na wananchi wote kuwa watulivu na kujihadhari na wanaotaka kuchafua Utumishi wa Umma Zanzibar kwa kutoa taarifa za uongo.

Kwa Taarifa hii, Tume ya Utumishi Serikalini haihusiki na lolote kuhusiana na taarifa hizo na inapenda kuwajuilisha kuwa nambari yake ya mawasiliano ya ofisi ni **0773 101012** ikiwa mtumishi au mwananchi atahitaji kuwasiliana nasi.

Ahsanteni.

Limetolewa na;

**KATIBU,**

**TUME YA UTUMISHI SERIKALINI,**

**S.L.P 1587,**

**Zanzibar.**

TUME YA UTUMISHI SERIKALINI
S. L. P 1587
ZANZIBAR